

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED



UFAFANUZI JUU YA KUONDOA CHANNELI ZA TELEVISHENI ZINAZOTAZAMWA BILA KULIPIA (FTA) KUTOKA VING'AMUZI VYA AZAM, MULTICHOICE NA ZUKU

1.0 UTANGULIZI

Utangazaji kwa njia ya televisheni una maudhui ya aina mbili. Maudhui yanayotazamwa bila kulipia (**FTA**) na maudhui yanayotazamwa baada ya mtazamaji kulipia kiasi fulani cha fedha kinachopangwa na mtoa huduma (subscription fee).

Wakati wa mfumo wa utangazaji wa analogia, vituo vya utangazaji vinavyorusha maudhui ya televisheni ya **FTA** kama vile **TBC1, CHANNEL TEN, ITV, STAR TV, CLOUDS TV** na **EAST AFRICA TV** ambavyo vilipewa leseni na Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (**TCRA**) ya kutangaza maudhui ya televisheni ya **FTA** vimetoa mchango mkubwa sana kwa Taifa kwa kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Wananchi wengi wa vipato vya chini, kati na juu wametumia mfumo huu wa **FTA** kufuatilia habari mbalimbali za kimaendeleo, siasa na uchumi. Hii inaonyesha umuhimu mkubwa wa **FTA** kwa jamii. Watu wengi wamefaidika na **FTA** kwa sababu gharama za kupata matangazo haya kwa mtazamaji ni nafuu na wananchi wengi wanazimudu. Mfumo wa **FTA** hufadhiliwa na matangazo ya biashara na taasisi mbalimbali zinazonunua 'airtime' kama vile Tanesco, National House, na wengine wengi ili kuviwezesha vituo vya Utangazaji kumudu gharama za uendeshaji. Upande wa mtazamaji, gharama halisi anayotakiwa kuona matangazo kwa mfumo wa **FTA** ni kuwa na chombo cha kupokelea matangazo tu yaani king'amuzi (decoder) stahiki.

Kwenye mfumo wa utangazaji wa dijitali, huduma za Televisheni za maudhui ya kulipia (**Pay TV**) kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini (Terrestrial) zilianza kupatikana. Hii ni kwa sababu ya uwezo unaopatikana kwenye teknolojia hii ya dijitali. Kwenye mfumo wa analogia, ilikuwa ni vigumu kuwa na maudhui ya kulipia kupitia mitambo iliyojengwa ardhini kutokana na mapungufu ya teknolojia hii. Baada ya Tanzania kuingia kwenye mfumo wa dijitali, utangazaji wa maudhui ya kulipia kupitia miundombinu ya ardhini (Digital Terrestrial Television) umewezesha kuwa na aina zote za maudhui ya **FTA** na maudhui ya kulipia (pay television). Awali mfumo wa maudhui ya kulipia ulikuwa unapatikana kwenye utangazaji kwa njia ya satellite tu.

2.0 UTANGAZAJI KWA NJIA YA DTT (DIGITAL TERRESTRIAL TELEVISION)

Utangazaji kwenye mfumo wa **Digital Terrestrial Television (DTT)** ni utangazaji wa maudhui ya televisheni unaotumia mitambo iliyojengwa ardhini. Mfumo huu umekuwa ukitumika kwa muda mrefu nchini na kuwa na watazamaji wengi kuliko mifumo mingine ya utangazaji. Hii ni kwa sababu bei za ving'amuzi vya **DTT** ni nafuu na wananchi wengi wanamudu kununua ving'amuzi (*decoder*) hivi. Baada ya kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa analogia kwenda dijitali, jukumu la kujenga mitambo na kurusha matangazo lilipewa kupitia leseni za kujenga miundombinu ya kubeba maudhui ya **FTA**, makampuni yajulikanayo kama Multiplex Operators au **MUX** kwa kifupi. Makampuni hayo na Ving'amuzi vyao ni:

KAMPUNI (MUX)	KING'AMUZI (DECODER) YAKE
Star Media (T) Ltd	StarTimes
Basic Transmission Ltd (BTL)	Continental
	DgiTek
Agape Associates Ltd (AAL)	Ting

Ili kuhakikisha kuwa mfumo huu wa **DTT** unaendelea kutoa huduma zake ipasavyo, **TCRA** iliweka miongozo ya ki-udhibiti kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanaendelea kupata huduma za **FTA** kupitia **MUX** kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- 2.1 Mfumo wa leseni ya **MUX** unawapa uwezo wa kusimika mitambo ya ardhini (**DTT**) na ile ya satellite (**DTH**) hivyo kuwawezesha wananchi wanaoishi mijini na vijijini kupata matangazo ya **FTA** bure na bila matatizo yoyote;
- 2.2 Kuweka kanuni na masharti ya leseni ambayo yatahakikisha kuwa huduma hii inalindwa ipasavyo kwa vile ina gharama nafuu na hutumiwa na watu wengi wenye vipato vya chini.
- 2.3 Vituo vya Utangazaji vilivyopewa leseni za **FTA** vinalazimika kutoa huduma hii kupitia miundombinu inayojengwa na **MUX** ili kuwajengea uwezo wa kusambaa nchi nzima.

3.0 UTANGAZAJI KWA NJIA YA SATELLITE (DTH)

Utangazaji kwa njia ya satellite ni mfumo unaotumika kutangaza maudhui ya kulipia (content by Subscription). Satellite hutumia mitambo ya kurushia matangazo iliyosimikwa angani hivyo kuwa na uwezo wa kufikia eneo kubwa la kijiografia. Kutokana na uwezo huo maudhui yanayotangazwa kwa njia ya satellite yamelenga kuwafikia watazamaji wanaoishi kwenye mabara (continent) mbalimbali duniani. Utangazaji kwa njia ya satellite umekuwepo kwa miongo kadhaa na mfumo wake wa kibiashara umelenga jamii zenye utamaduni na mila tofauti. Maudhui yanayorushwa kupitia satellite huwekwa kwenye vifurushi tofauti kwa kutegemea mahitaji ya kila nchi na kusambazwa kwenye maeneo tofauti. Hivyo basi maudhui yanayotazamwa kupitia mfumo wa utangazaji wa satellite ni maudhui ya kulipia (content by Subscription). Vilevile Utangazaji wa satellite unahitaji kuwa na madishi ya kupokelea matangazo ambayo huhitaji nafasi ya kutosha kuyasimika. Watanzania wengi wanaoishi mijini kwenye nyumba za kupanga wamekuwa na changamoto ya kusimika madishi haya ili waweze kuangalia matangazo kwenye mfumo wa satellite hivyo kupendelea utangazaji unaotumia **antenna** za mitambo ya ardhi zisizotumia nafasi kubwa na zina gharama nafuu.

3.1 MASHARTI YA LESENI YANAYOHUSU FTA

Maudhui ya **FTA** yamebeba vipindi vingi vyenye umuhimu kwa jamii kama vile Taarifa za Habari, matukio (current affairs), vipindi vya watoto, na habari nyingi zinazohusu jamii na maendeleo kwa ujumla. Ili kuendelea kulinda maudhui ya utangazaji kwenye mfumo wa **FTA**, Masharti ya leseni yametolewa yanayohakikisha kuwa watazamaji wanaona matangazo ya **FTA** bila kulipia. Masharti hayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa maudhui ya **FTA** hayawekwi kwenye majukwaa (satellite platform) ambayo leseni zao ni kwa ajili ya maudhui ya kulipia. Kanuni za Radio na Televisheni za Mawasiliano ya Ki-elektroniki na Posta za 2018, zinawataka vituo vya Utangazaji vyenye leseni za **FTA** kuhakikisha kuwa maudhui yao yanaonekana bila kulipia na yanabebwa na watoa huduma wa **MUX**.

3.2 MASHARTI YA LESENI YALIYOPO KWA WATOA HUDUMA KUPITIA VING'AMUZI VYA AZAM, MULTICHOICE NA ZUKU

Watoa huduma za maudhui kupitia ving'amuzi vya **AZAM, MULTICHOICE** na **ZUKU** waliomba leseni ya 'Support Services for Subscription Television Content Services by Satellite' na kupatiwa kama walivyoomba. Neno 'Subscription' limetafsiriwa kwenye Kanuni za Radio na Televisheni za Mawasiliano ya Ki-elektroniki na Posta za 2018, kifungu cha kwanza kama maudhui yanayotazamwa kwa kulipia. Majukumu ya mwenye leseni hii yameainishwa kwenye kifungu cha saba (7) ikiwa ni pamoja kutoa huduma kwa wateja wao ambao wateja hao wametambuliwa kama 'Subscribers'. Tafsiri ya neno 'Subscriber' limeainishwa kwenye Kanuni hizo kifungu kilekile cha kwanza kuwa ni wateja ambao wamejiunga kwenye mtandao kwa ajili kupatiwa huduma za maudhui ya kulipia. Hivyo basi kwa kuzingatia masharti ya leseni waliyopewa, ubebaji wa maudhui ya FTA na kuyalipisha ni kinyume na madhumuni ya huduma ya leseni walizonazo.

4.0 HITIMISHO

- 4.1** Kulipisha maudhui ya **FTA** ni kwenda kinyume na Kanuni na Sheria zilizopo kwani Watanzania wengi wenye vipato vya chini na kati wanategemea sana mfumo wa utangazaji wa **FTA** ambao unawezesha kupata taarifa za Habari na Matukio mbalimbali (current Affairs) kutoka kwenye jamii.
- 4.2** Kuendelea kurusha matangazo ya **FTA** na kuyapokea kupitia ving'amuzi vya **AZAM, ZUKU** na **MULTICHOICE** ambapo maudhui yake yanapokolewa kupitia majukwa ya maudhui ya kulipia ni kwenda kinyume na Kanuni na masharti ya leseni zao.
- 4.3** Kulipisha maudhui ya **FTA** ni kuwanyima haki watoa matangazo ya biashara ambao wanalipia fedha nyingi ili wananchi wengi kupitia mfumo wa kutazama televisheni bila kulipia waweze kuona bidhaa zao na kuzinunua.
- 4.4** Usimamizi wa utekelezaji wa masharti hayo mbali na kutumia mamlaka ya kiudhibiti unahitaji uungwaji mkono wa wadau mbalimbali.